# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SHUGHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

# IDARA YA KILIMO

## UTANGULIZI

- Wilaya ina jumla ya wataalam 82 walioko ngazi ya kijiji, 27 ngazi ya kata na 9 makao makuu ya wilaya.
- Wilaya imeweka kipaumbele katika mazao ya pamba, alizeti, mpunga, na mtama. Wataalam hao hushirikiana na vikosi kazi ngazi ya vijiji, kata na wilaya katika kutoa ushauri wa mbinu bora za kilimo.

# MAFANIKIO

## KILIMO CHA PAMBA

- Kwa msimu huu (2016/2017), Wilaya imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa pambakwa 143% toka kilogramu **426,200** (tani 426.2) msimu wa **2015/2016** hadi kilogramu **1,037,000** (tani **1,037)**.

- Mafanikio hayo yametokana na utekezaji wa kilimo cha mkataba na usimamizi wa pamoja wa zao la pamba katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na vijiji kupitia vikosi kazi vilivyoundwa ngazi ya Wilaya, kata na vijiji. Pia mafanikio hayo yalichangiwa na usambazaji pembejeo kwa wakati mbegu (tani 300.19, viuatilifu chupa 22,000 na vinyunyizi 150) katika vijiji vya Misungwi. Asilimia 99 ya wakulima walio lima pamba walikopeshwa pembejeo.

# Inaendelea

- Halmashauri inatarajia kupata ushuru wa wa pamba kiasi cha **Tsh. 62,220,000/=**. Kwa uzalishaji huo jumla ya Tsh. **1,244,400,000/=** zimeingia kwenye mzunguko kupitia wakulima wa pamba ambapo nihatua nzuri katika kudhibiti mdororo wa uchumi miongoni wa wananchi.

- Katika jitihada za kufufua zao hilo, Wilaya iliweza kupata ushirikiano Mkubwa wa kitalamu na wa kisheria kutoka Bodi ya Pamba, Gatsby Africa na katika makampuni (ICK Cotton Oil Company Ltd).

***Picha Na. 1 ,chini:***

*Wataalam walipomtembelea Mzee Balele Lutaligula (Katikati) Kijiji cha Lubili aliyevuna Pamba kl 15,705*



***Picha Na.2, chini:***

*Shamba la Mkulima Busweke Kulwa (Mapilinga)-Aina ya mtama ni:  MTAMA NACO I*



***Picha Na.3, chini:***

*Shamba la Mkulima Samweli Busagala (Mapilinga) –*

*Aina ya mtama ni:* ***HAKIKA***



# Inaendelea

- Wilaya ilinunua kilo 1,625 za mtama kwa thamani ya Shs 6,500,000/= na kuwauzia wakulima kwa bei ya Shs 4,000/= kwa kilo. MRHP ilisambaza kilo 100, Hope II ilisambaza kilo 113, Wauzaji wa pembejeo walisambaza kilo 1,262. Jumla Kuu ya mbegu bora ya mtama iliyosambazwa kwa Wilaya ni Kilo 3,000. Mbegu iliyopandwa ni kilo 895.5. Ekari zilizopandwa ni Ekari 447.75. Mavuno ya mtama msimu 2016/2017 ni Tani 1226.6. Akiba ya mbegu ni kilo 2,104.5 ambazo zitapandwa msimu 2017/18.

- Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kushirikiana na Mradi wa kuwajengea uwezo wataalam wa umwagiliaji awamu ya pili- TANCAID II na Mradi wa kutekeleza miradi midogo ya umwagiliaji awamu ya tatu- SSIDP III ilisitisha kuanzisha miradi mipya ya umwagiliaji na badala yake wakamilishe kwanza miradi yote iliyokuwa imeanzishwa haikukamilika ikasimama ujenzi wake.

# ZAO LA ALIZETI

- Wilaya ilinunua tani sita (6) kwa kwa thamani ya Shs 9,000,000 na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa “Kopa mbegu lipa mbegu”. Kilo zilizopandwa ni 4,500 sawa na ekari 1,500. Kilo 1,500 hazikupandwa kutokana na ukame. Akiba ya kuanzia ni Kilo 1,500. Zao la alizeti litakuwa ni zao la biashara kuliko kutegemea zao moja tu la pamba.

# KILIMO CHA UMWAGILIAJI

- Wilaya ina eneo la hekta 8,969 linalofaa kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji. Jumla ya hekta 1,009.5 tu ndiyo zinazotumika kwa kilimo cha Umwagiliaji kwa sasa.

# Inaendelea

- Kwa hiyo Serikali imeagiza kuwa miradi yote ya zamani itakayokamilishwa na ile mipya itakayoanzishwa ni lazima ifuate "Mwongozo Kabambe wa Umwagiliaji" Wilaya inao wataalam wawili ambao wamepata mafunzo ya matumizi ya Mwongozo Kabambe wa umwagiliaji na wanaweza kuibua miradi ya umwagiliaji hadi kufikia utekelezaji wake.

# Inaendelea

**Wilaya imeanza kutekeleza agizo hilo kama ifuatavyo:-**

- Kuanzia mwaka jana Novemba 2016 hadi Februari 2017 Wataalam wa wilaya na Umwagiliaji Kanda kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji(NIRC) na JICA wamefanya na kukamilisha Zoezi la Uibuaji miradi kwa hatua zote 12 kwenye Skimu ya Igenge. Pia tayari andiko la kuomba fedha za kukamilisha ujenzi wa skimu limeshaandikwa kupitia kwa Mhandisi wa Umwagiliaji Kanda-Mwanza na kutumwa Wizarani.

- Mipango mingine iliyopo ni kufanya Zoezi la Uibuaji kwa Miradi iliyobakia ya Igongwa, Nyambeho, Nyashidala na Mbarika ili nayo iweze kuandikiwa andiko la kupata fedha za kuikamilisha.

***Picha Na.4, chini:***

*Wataalam kutoka Wizarani, JICA, ZIO, Wilayani na Wakulima wakitembelea eneo la Mradi wa umwagiliaji Igenge.*



*Wizarani, JICA, ZIO, na Wilayani wakitoa mafunzo ya Uibuaji wa Miradi kwa wakulima wa mradi wa umwagiliaji Igenge.*



# Inaendelea

- Mafanikio haya yamesababishwa na ushirikiano kati ya vikosi kazi vya vijiji, kata na Wilaya. Kwa msimu huu wilaya itahakikisha inajitosheleza kwa chakula chini ya mpango kabambe wa kutokomeza njaa Misungwi ambapo wataalam na viongozi wote watashiriki katika kutekeleza mpango huu.

# IDARA YA MIFUGO

## UTANGULIZI

Wilaya ina jumla ya wataalamu 49, kati ya hao maafisa mifugo 7 wapo wilayani na maafisa uvuvi 03 wapo wilayani. Watumishi 03 wapo ngazi ya Tarafa kwa upande wa uvuvi, na 27 wapo ngazi ya kata kwa upande wa mifugo na waliobaki 09 wapo ngazi ya vijiji. Majukumu muhimu ya idara ya mifugo kipindi hiki yalikuwa ni kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora wenye tija na pia kuhakikisha wanafuga mifugo kulingana na ukubwa wa maeneo yaliyopo; idara imesisitiza wafugaji kupunguza idadi ya mifugo yao ilikubaki na mifugo michache yenye tija.

# MAFANIKIO YALIYOFIKIWA KWA MWAKA 2016/2017

1. Ukarabati wa machinjio ya Misungwi kwa kujenga uzio na choo. Jumla ya Tshs 10,000,000 .00 zilitumika na ujenzi umekamilika.

***Picha Na.1,chini:*** *Choo katika machinjio ya Misungwi kikiwa katika hatua ya Ukamilishaji*



# Inaendelea

2. Ujenzi wa machinjio mpya ya Usagara, jumla ya Tshs 10,000,000.00 zimetolewa,msingi umekamilika, jamvi limeshawekwa na ujenzi uko katika hatua ya kumalizia kuweka nguzo zote.

3. Kufunguliwa na kuanza kwa mnada wa upili wa Nyamatala unaofanyika mara sita kwa juma,na gulio la kila jumanne.

4. Utambuzi, usajili na upigaji chapa wa ng’ombe. Wafugaji 6,200 wameshasajiliwa na Ng’ombe 72,428 wamesha sajiliwa kutoka kata 21 kati ya 27. Zoezi la upigaji chapa limekwishafanyika kwa majaribio katika vijiji vya Mwambola na Ngudama. Uzinduzi rasmi umepangwa kufanyika mwezi wa Agosti.

***Picha Na.2,chini:***

*Ngo'mbe waliopigwa chapa kijiji cha Ngudama (TMSG 068)*



**Inaendelea**

5. Mafunzo ya ufugaji kwa kushirikana na chuo cha mafunzo Mabuki na Taasisi ya utafiti wa mifugo Mabuki. Wafugaji 40 wamepeshapatiwa mafunzo ya ufugaji wa ng’ombe wa maziwa, 7 wamepata mafunzo ya unenepeshaji wa ng’ombe na uzalishaji pamoja na hifadhi ya malisho, wafugaji 88 wamepewa mafunzo ya uzalishaji wa kuku chotara na kugaiwa vifaranga 3250 katika vijiji vya mwambola, nguge, Mabuki na Kijima.

6. Kuongezeka kwa mifugo inayoogeshwa na kupungua kwa magonjwa yaenezwayo na kupe kutoka asilimia 25 hadi 10.

***Jedwali Na.1:***

*Idadi ya mifugo iliyoogeshwa*

| Aina | Ng’ombe | | Mbuzi | | Kondoo | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Josho | Bomba | Josho | Bomba | Josho | Bomba |
| Jumla | 62,147 | 40,124 | 32,059 | 18,390 | 11,885 | 13,384 |

***Picha Na.3,chini:***

*Mifugo ikiwa katika josho la Mwalogwabagole-Bulemeji*



# Inaendelea

7. Chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mifugo kuku 32,543 walichanjwa kuzuia kideri 3,457 kuzuia ndui, Ng’ombe 31,248 walichanjwa kuzuia chambavu na mbwa 2,340 walichanjwa kuzuia kichaa cha mbwa.

# ELIMU MSINGI

| Na | SHUHGULI/LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 1 | Uandikishaji wa watoo wa elimu ya awali kwa asilimia mia | Tumefanikiwa kuandikisha watoto wote rika lengwa wapatao 13170 sawa na 99.8% kujiunga na madarasa ya awali. |
| 2 | Uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa std I-2017 | Tumefanikiwa kuandikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wapataao 18404 sawa na 99.9% kuanza STD I - 2017. |

| Na | SHUHGULI/LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 3 | Ujenzi wa vyoo katika shule 24 vyenye matundu 296 | Tumfanikiwa kukamilisha vyoo 2 vyenye matundu 16 vimekamilika na vyoo 22 vyenye matundu 280 katika shule 22, ujenzi wake unaendelea kwa lengo kupunguza msongamano wa watoto wakati wa kupata huduma ya choo. |
| 4 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 15 katika shule za msingi 4 (Mbela, Mitindo, Busagara, Kigongo, Misungwi) | Tumefanikiwa kujenga vyumba 15 vya madarasa kashule za msingi Mbela , Mitindo ,Busagara, Kigongo na Misungwi kwa lengo la kupunguza msongamano ya wanafunzi darasani. |

# Inaendelea

| Na | SHUHGULI/LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 5 | Utengenezaji wa madawati na kuondoa tatizo la wanafunzi kukaa chini mahitaji yalikuwa 34,677. | Tumefanikwa kutengeneza madawati 35252 sawa na 102% katika mahitaji ya adawati 34,677 na kuwa na ziada ya madawati 575 ili kuondoa tatizo la wanafunzi kukaa chini. |
| 6 | Kuandaa takwimu mbalimbali za shule za msingi na kuziingiza kwenye mfumo wa wizara | Tumefanikiwa kukusanya takwimu mbalimbali za walimu, wanafunzi , samani na miundo mbinu toka shule zote za msingi na kuziingiza kwenye mfumo |

# ELIMU SEKONDARI

| Na | LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 1 | Kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya SEDP katika Shule za Sekondari. | Tumefanya ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu katika shule za Nyabumhanda,Shilalo na Ilujamate. |
| 2 | Kukagua ufundishaji wa walimu ajira mpya ili wathibitishe kazini kuthibitisha walimu ajira walimu 78. | Walimu ajira mpya walikaguliwa na waliokidhi vigezo wameandikiwa barua za kuthibitishwa kazini.Jumla ya walimu 76 wamethibitishwa kazini. |

| Na | LENGO | MAFANIKIO |
| --- | --- | --- |
| 3 | Kufanya ufuatiliaji wa shughuli za ufundishaji wa walimu 546 mashuleni. | Tumefanya ufuatiliaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji katika shule zote 23 za Sekondari.Ufundishaji umefanyika vizuri. |
| 4 | Kutoa vitendea kazi kwa maafisa 5 wa Idara ya Elimu Sekondari | Tumefanikiwa kununua vitendea kazi vya ofisi ambavyo ni Computa 2 (laptops) kwa kutumia fedha za P4R. |

# Inaendelea

| Na | LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 5 | Kuandaa takwimu mbalimbali za Shule za Sekondari na kuziingiza kwenye mfumo wa Wizara. | Tumekusanya takwimu za idadi ya wanafunzi, walimu,miundombinu na samani toka shule zote za sekondari na kuziingiza kwenye mfumo wa Tamisemi. |
| 6 | Kukarabati vyumba vya madarasa katika shule za sekondari. | Tumefanikiwa kufanya ukarabati wa Madarasa 2 katika Shule ya Sekondari Paul Bomani na vyumba 2 Shule ya Sekondari Shilalo kwa kutumia fedha za SEDP II na Fedha za P4R. |

| Na | LENGO | MAFANIKIO |
|---|---|---|
| 7 | Kupandisha Kiwango cha Ufaulu wa wanafunzi katika Mitihani ya Kitaifa. | Tumefanikiwa kupandisha kiwango cha ufaulu kwa Shule zetu za Sekondari toka asilimia 71 kwenda asilimia 75.3 na kuchukua nafasi ya 3 ki mkoa kwa matokeo ya mtihani. |
| 8 | Kutengeneza samani katika shule 23 za sekondari. | Tumefanikiwa kutengeneza madawati kwa shule za sekondari na kukamilisha mahitaji ya wanafunzi wapatao 10696 na kubaki na akiba ya madawati 588. |

# IDARA YA AFYA

**UTANGULIZI**

- Idara ya afya ina jumla ya vitengo 8 ambavyo ni; Utawala, Afya kinga, Dawa, Maabara, Meno, Uuguzi, na kitengo cha Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, vitengo hivyo hufanya kazi kwa kushirikiana na vitengo vidogo (section) mbali mbali ambavyo vinaratibiwa na waratibu husika. vitengo hivyo ni: Afya ya Mama na Mtoto, Afya Mashuleni, TB, Afya ya Jamii, Lishe, HIV/Ukimwi, Tiba asili, Takwimu, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa, Mfuko wa Bima ya afya ya Jamii, Malaria, na kitengo cha TB&Leprosy.

- Katika mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya Tsh 259, 613,707 kutoka mfuko wa pamoja (HSBF) zilipangwa kwa manunuzi ya madawa na vitendanishi ambapo fedha zote (100%) zilipokelewa na kutumika. Hata hivyo kiasi cha Tsh 121,368, 651 fedha ya bakaa ilitumika kununua madawa na vitendanishi. hivyo, jumla ya fedha iliyotumika kununua madawa na vitendanishi kwa mwaka 2016/2017 ni Tsh 380,982,358.

- Katika kutekeleza mpango wa afya (CCHP) 2016/2017 Idara ilipanga kutumia vyanzo mbalimbali katika kununua madawa na vitendanishi. Nyanzo hivyo ni pamoja na Mfuko wa afya wa pamoja (Basket Fund) na ruzuku ya madawa kutoka serikali kuu (Recipt in Kind).

# MAFANIKIO;

- Jumla ya fedha zilizopangwa kwa mfuko wa busket fund ni 797, 577,000 ambapo zote zimepokelewa na zimetumika Tsh 741, 858,757, Fedha zilizobaki ni Ths 55, 718,243 ambazo zimevuka mwaka hivyo zitatumika kwa mwaka wa fedha 2017/18 kama fedha za bakaa.
- Aidha jumla fedha ya ruzuku ya dawa (receipt in kind) ilipangwa kiasa cha Tsh 485, 579,916 ambapo fedha zote zimepokelewa na Tsh 263, 485,838.27 sawa na 54.26% zimetumika. Hali ya upatikanaji wa dawa MSD ni 96.6%

# RBF

- Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 idara ilipokea jumla ya Tsh 410,000,000 kama fedha ya kuanzia (status fund) ambapo zote zimetumika kwenye ukarabati wa vituo husika vilivyoingiziwa fedha hizo.

- Aidha, Jumla ya Tsh 463,283,252.50 fedha za mfuko wa malipo kwa ufanisi zilipokelewa ambapo tsh 115,820,813 sawa na 25% ya fedha zilizopokelewa zilitumika kwa ajili ya kutoa motisha kwa wafanyakazi kwa mujibu wa muongozo wa matumizi ya fedha za RBF. na Tsh 347,462,439.50 sawa na 75% zilitumika kwa matumizi mbali mbali ikiwemo ukarabati vituo na manunuzi ya dawa na vifaa tiba.

## Idara ya afya kwa mwaka 2016/2017 ilipanga kutekeleza miradi/shughuli mbalimbali kama ilivyobainishwa hapa chini:-

### 1. Utawala

Idara ilipanga kujenga zahanati 2 (Nyang'homango na Lutalute) ambapo zote zimekamilika.

### 2. Mama na Mtoto

Idara ya afya ilipanga Kuboresha Huduma ya afya ya uzazi na mtoto kwa kuhamasisha akinamama 14,561 kuhudhuria kliniki.  hata hivyo, Jumla ya akinamama 18,149 walihudhuria kliniki sawa na 124% ya lengo wamehudhuria clinic.

# Inaendelea

Vile vile idara ilipanga kuhamasisha na kupima maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa wanawake wajawazito 14,561 ambapo Wanawake wajawazito wamehamasika na Upimaji umefanyika kwa wajawazito 17,386 sawa na 10*2%* na waliokutwa na maambukizi ni 380.

**3. Malaria**

- Katika kupambana na ugonjwa wa malaria, idara imepanga Kupunguza uwepo wa malaria katika wilaya kutoka 29% mpaka 25% ambapo hadi sasa Uwepo wa malaria umepungua kutoka asilimia 29 hadi 26.4. hii ni sawa na 91% ya lengo.
- Pia katika kuboresha huduma za mama na mtoto, idara ilipanga Ugawaji na usambazaji wa vyandarua kwa wanawake wajawazito 14,561 ambapo Wanawake wajawazito 14 487 sawa na 99.4% wamepata vyandarua.

# Inaendelea

## 4. Lishe

- Katika kutatua tatizo la utapia mlo, Kutoa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka 5 ambapo watoto 148,447 walipaswa kupata Huduma hii. Hata hivyo Watoto 152,198 sawa na 102% wamepata dawa za minyoo na Matone ya Vitamin A.

## 5. Dawa Na Vifaa Tiba

- Idara ilipanga Kununua dawa na vifaa tiba na kusambaza vituo 46 ambapo Dawa na vifaa tiba vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo 46. Katika vituo vyote vya afya na zahanati dawa zinapatikana kwa 96.6%.

# Inaendelea

## 6. Afya ya Jamii

- Katika kuimarisha huduma ya afya ya jamii, idara ilipanga Kutoa mafunzo kwa watoa Huduma ngazi ya jamii 148 ili kukabiliana na vifo vitokanavyo na uzazi. Hata hivyo, Watoa Huduma ngazi ya jamii 148 sawa na 100% wamepata mafunzo na watafanya kazi ya kuhamasha jamii kufika na kutumia Huduma za afya vituoni na hatimaye kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

# Inaendelea

## 7. Afya Mashuleni

- Kufanya uchunguzi kaika shule za msingi nane katik kata ya misungw, kijima, shilalo, na nhundulu katika shule za kijima, misungwi, mwagiligili mwamagili mwamboku, Isakamawe, Mwawile, na Ikoma. Hata hivyo, Watoto 4032 sawa na 75% kati ya wanafunzi 5353 walipimwa.
- Vilevile, idara ilipanga Kuboresha usafi wa mazingira ya shule katika katika shule 146 kwa kutembelea shule zote ili kutoa elimu ya usafi wa mazingira. Shule 11 sawa na 8% kati ya shule 146 zimetembelewa na elimu ya usafi wa mazingira imetolewa.

# Inaendelea

## 8. Afya ya Kinywa na Meno

- **Idara ilipanga** Kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba ya kinywa na meno kutoka 60% had 100%. hata hivyo idara imefanikiwa Kuongeza upatikanaji wa vifaa (seti za kutolea huduma ya kinywa na meno) kwa kununua seti 3 kati ya nne sawa na 75% ya lengo.
- **Vile vile, idara ilipanga** Kutoa huduma ya kinywa na meno kwa wagonjwa wanaohudhuria katika kliniki ya meno katika hospitali ya wilaya. Wagonjwa 949 sawa na 100% ya waliofika katika kliniki ya meno wamehudumiwa na kupatiwa elimu ya afya.

# Inaendelea

## 9. Chanjo

**Katika kuimarisha huduma za chanjo kwa mama na mtoto:**

- Tumefanikiwa kutoa chanjo kwa watoto 15,845 sawa na asilimia 100%.
- Pia Tumefanikiwa kutunza mnyororo baridi vituoni kwa kugawa mitungi 3 kila kituo na mtungi mmoja wa kuchemshia.
- Tumedhibiti uhamishaji wa chanjo kutoka kituo kimoja kwenda kingine kwa sababu za kuishiwa nishati ya gesi vituoni.
- Tumefanikiwa kuboresha huduma za chanjo na kuzifanya kuwa huduma za msingi na mhimu kwa jamii zetu na hatimaye kupenda huduma zetu.

- Tumefanikiwa kuongeza huduma za mikoba na mobile clinic kutoka safari 444 zilizokuwa zimepangwa kwenye mpango mpaka kufikia safari 1,241 hii imesadia kufikia malengo yetu.

# Inaendelea

## 10. Afya Kinga

- Idara ilipanga Kuongeza asilimia ya kaya zenye vyoo bora kutoka 17% hadi 50 %. Hata hivyo, kaya zenye vyoo bora zimeongezeka kutoka 17% hadi 34%.

# IDARA YA MAJI

- **UTANGULIZI**
- Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri kupitia Idara ya Maji iliidhinishiwa Bajeti ya jumla ya fedha Tshs. 2,551,858,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Progammu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP). Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilipokea kiasi cha fedha cha Tsh. 740,191,664.69 kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Bakaa ya Tshs. 493,884,198.45 na kuleta jumla ya Tshs.1, 234,075,863.14

## Inaendelea

- Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017 Halmashauri kupitia Idara ya Maji ilitumia kiasi cha Tshs. 922,674,724.06 kwa ajili ya kulipa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya Maji, Mhandisi Mshauri (COWI Tanzania) na Usimamizi na ufuatiliaji ujenzi wa Miradi ya Maji pamoja na uundaji na usajili wa vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs).
- Aidha Idara ya Maji imefunga mwaka ikiwa na Bakaa ya Tshs.311,401,139.08 ambazo ni fedha za Madai ya Wakandarasi na uhamasishaji, uundaji na Usajili wa

# MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2017 Idara imefanikiwa kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

- **Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Mradi wa Maji bomba Fella**
- Kufanya ukarabati wa visima vya kina kirefu katika vijiji vya Mitindo (Hospitali ya Mitindo), Mondo 1 (Mwaniko sekondari), Mwambola 1(Kitongoji cha Budutu) Nyamatala 1,Usagala 1(Misungwi), Gambajiga 1, Nange 1, Mitindo A 1, Kanyelele 1, Mbarika (mradi wa Maji bomba), Ngaya Ngaya 1, Ng'ombe 2, Misungwi Mitindo 1,Milembe Sekondari 1, Kasololo 1, Ngudama 1, Gambajiga 2, Mwaniko 1, Lubuga 1, Mbela 1 na Misungwi B 1 na kurejesha huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo husika.

# Inaendelea

- Kwa kushirikiana na Mashirika ya kidini tumefanikiwa kuchimba visima virefu na vifupi katika vijiji vya Kasololo visima 6, Isuka kisima 1, Kifune kisima 1, Lukanga kisima 1, Usagala kisima 1, Ngereka kisima 1, Ibongoya B visima 2 na Songiwe kisima1.
- Tumefanikiwa kuchimba kisima kirefu na kufunga pampu ya umeme katika shule msingi maalum (Mitindo) kwa fedha za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi na Kisima hicho kimekamilika kuchimbwa na kinatoa huduma ya maji safi na salama kwa watoto wa shule maalum ya Mitindo. Pia tumesimamia ujenzi wa matenki ya kuhifadhi maji na ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji katika shule hiyo.

# Inaendelea

- Tumefanikiwa kuunda vyombo/Jumuiya za Watumiaji Maji vijijini vya Kasololo, Sumbugu, Matale, Ngaya, Igenge, Mwawile, Isenengeja, Lubili, Ilalambogo na Nyamatala.
- Tumefanikiwa kupata fedha za kulipa madeni ya wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Igenge, Ngaya, Matale, Manawa na Misasi.
- Tumefanikiwa kupata fedha kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili kujenga miundombinu ya umeme kwenye chanzo cha Maji mradi wa maji Fella.

# Inaendelea

- Tumefanikiwa kuandaa makisio ya gharama ya mradi wa maji wa Mbarika – Ngaya na kukiwezesha kitengo cha manunuzi kutangaza ili kupata mkandarasi wa kutekeleza mradi huo.
- Tumefanikiwa kuunganisha miundombinu ya mradi wa umwagiliaji na mradiwa wa usambazaji maji katika kijiji cha Mbarika.
- Tumefanikiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa mbali mbali za Idara pamoja na kuandaa Mpango wa Bajeti ya mwaka ujao wa 2017/2018 , maandakiko mbalimbali ya miradi ya Programu ya Maji vijijini na Mpango Mkakati wa miaka 5 kuanzia mwaka fedha 2016/17 mpaka 2020/2021.

# IDARA YA UJENZI

Halmashauri ina mtandao wa barabara wenye jumla ya Km 924 ambao umegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni;-

1. Barabara Kuu (Trunk Roads) zenye urefu wa Km. 53
2. Barabara za Mkoa (Regional Roads) zenye urefu wa Km.167
3. Barabara za Wilaya na Vijijini (District and Feeder Roads) zenye urefu wa Km.704

# MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MATENGENEZO YA BARABARA

Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilipanga kufanya matengenzo ya barabara katika makundi manne ambayo ni matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu Korofi, Matengenezo ya kipindi maalumu pamoja na kujenga Makalvati na kufanikiwa kutekeleza kazi hizi za mwaka wa fedha 2016/2017 kwa asilimia 45.

# Inaendelea

1. **Matengenezo ya kawaida (Routene maintenance);**

Halmashauri ilipanga kutengeneza barabara yenye urefu wa Km.56.1 kwa gharama ya Tshs.56,100,000/=, hadi sasa halmashauri imefanikiwa kuchongwa jumla ya Km. 51.36 kwa gharama ya Tshs.51,350,000/=, hata hivyo ilipanga kumwaga cgangarawe m3 10,990 kwa gharama ya Tshs.120,890,000/= hadi sasa changarawe m3 7,380 zimemwagwa na kusambazwa ambayo imegharimu kiasi cha Tshs.81,180,000/=

2. **Matengenezo ya sehemu Korofi (Spot Improvement);**

Halmashauri ilipanga kutengeneza barabara yenye urefu wa Km.8.45 kwa gharama ya Tshs.16,900,000/=, Kujenga mitaro ya pembeni mwa barabara m3 379, kwa gharama ya Tshs. 32,215,000/= na kuchimba mitaro ya kukinga na kutupa maji m3 11,576 kwa gharama ya Tshs.46,304,000,hadi sasa jumla Km.6.2 zimelimwa kwa gharama ya Tshs.12,400,000/=, m3 130 za mitaro imejengwa kwa gharama ya Tshs.11,050,000/= na m3577 zimechimbwa kwa gharama ya Tshs.2,308,500/=,

# Inaendelea

**3. Matengenezo ya kipindi maalumu ( Periodit Maintanance);**

- Halmashauri ilipanga kufanya matengenezo ya barabara yenye urefu wa Km.20 kwa gharama ya Tshs.40, 000,000/=, hadi sasa jumla ya Km.12zimetengenezwa kwa gharama ya Tshs.24, 000,000/=

**4. Ujenzi wa Makalvati;**

- Halmashauri ilipangwa kujenga jumla ya Makalvati ya njia 51 kwa gharama ya Tshs.171, 000,000/= ambapo hadi sasa jumla ya makalvati ya njia 14 yamejengwa kwa gharama ya Tshs.42, 000,000/=

# IDARA YA ARDHI

**MAFANIKIO KWA MWAKA 2016/2017**

1. Kiasi cha Tshs.321, 317,613.47 kimekusanywa ikiwa ni makusanyo ya maduhuri ya kodi ya Ardhi kati ya 130,000,000/= zilizokuwa zimepangwa kukusanywa kwa mwaka.

2. Hati 202 za maeneo ya mjini zimeandaliwa kati ya hati 100 zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka na Hati 10 za kimila kati ya 50 zimeandaliwa.

3. Malalamiko 38 yameshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kati ya malalamiko 44 yaliyopokelewa.

4. Eneo la uwekezaji Nyang'homango lenye ukubwa wa Hekta 2400 limebainishwa.

# Inaendelea

5. Viwanja 618 vimepimwa katika maeneo ya kata za Fela, Misungwi, Idetemya na Usagara kati ya Viwanja 400 vilivyokuwa vimepangwa kupimwa kwa mwaka.

6. Michoro 15 ya mpango miji imeandaliwa kati ya michoro 17 iliyokuwa imepangwa kuandaliwa kwa mwaka 2016/2017. Michoro hiyo ipo katika maeneo ya Misungwi michoro2, Usagara michoro3, Idetemya michoro 2, Nyang'homango michoro 4, Nyashishi michoro 2, Ngudama michoro 3 na Mayolwa michoro 3.

7. Eneo la bandari ya Nchi kavu limetengwa lenye ukubwa Ekari 1000 katika eneo la Fela ambapo tayari wananchi wamelipwa fidia.

# IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

## UTANGULIZI

Idara ya Mandeleo ya Jamii ina jumla ya vitengo 04 ambavyo ni Utafiti, Mipango naTakwimu, Kitengo cha UstawiwaJamii, Kitengo cha UKIMWI, Pamoja na Kitengo cha Wanawake, Jinsia na Watoto. Idara ina jumla yawatumishi 17

# MAFANIKIO YALIYOFIKIWA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JULAI, 2016 HADI JUNI, 2017:-

Katika kipindi cha Kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Juni 2017, Idara imeweza kufikia mafanikio yafuatayo:-

1. Vikundi 06 vya Wanawake vimepatiwa mkopo wenye thamani ya Tsh.25,600,000/= kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF).Vikundi hivyo ni:-

- Huruma Idetemya Tsh.5,000,000/=
- Buyegi Women Group-Usagara Tsh.5,000,000/=
- Juhudi Ngudama Tsh.4,600,000/=
- Wapendanao ‘C’ Kanyelele Tsh.5,000,000/=
- Akina Mama Wachapakazi-Lukelege Tsh.3,000,000/=
- MTAWAMA-Mamaye Tsh.3,000,000/=

# Inaendelea

2.Vikundi 03 vyaVijana vimepatiwa mkopo wenye thamani ya Tsh.20,600,000/=, kati ya fedha hizo, kiasi cha Tsh.5,000,000/= zilikopeshwa kwa Kikundi cha Mayanasi, ikiwa ni Mchango wa Halmashaurina Tsh.15,600,000/= zilitolewa na Wizara kwaVikundi vya Umoja wa Chama cha Waendesha Pikipiki Misungwi Ts.9,600,000/= naVijana Kwanza Usagara Tsh.6,000,000/=.

# Inaendelea

3. Vikundi 06 vimepatiwa mkopo wa Mpango wa SLEM wenye jumla ya Tsh.31, 000, 000/=. Vikundi hivyo ni:-

- Tumaini Ngaya Tsh.5,000,000/=
- Vijana Computer-Koromije Tsh.5,000,000/=
- Uchumi Ibongoya 'A' Tsh.5,000,000/=
- Umoja Misasi Center Tsh.5,000,000/=,
- Mshikamano Gemedu Tsh.5,000,000/=
- Mkombozi Wood Factory-Misungwi Tsh.6,000,000/=

4. Jumla ya Vikundi 108 vimesajiliwa, kati ya vikundi hivyo, Vikundi 72 vimefanikiwa kufungua Akaunti Benki.

# Inaendelea

5. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa Vikundi vya Wanawake naVijana. Vikundi 27 vya Wanawake na Vijana vimefanyiwa ufuatiliaji kwa lengo la kuhimiza marejesho ya mkopo. Kiasi cha Tsh. 31,934,254/= kimerejeshwa

- Tsh.21,350,904/= nimarejesho ya Vikundi vya Wanawake
- Tsh.10,858,350/= nimarejesho ya Vikundi vyaVijana

6. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa Vikundi vya kiuchumi na uzalishaji mali. Vikundi 13 vilivyokopa fedha ya Mfuko wa SLEM Vimefanyiwa ufuatiliaji kwa lengo la kuhimiza marejesho ya mkopo. Kiasi cha Tsh. 19,141,665/= kimerejeshwa.

# Inaendelea

7. Kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuliza Maendeleo. Uhamasishaji umefanyika katikaVijijivya Mhungwe na Lubuga vilivyopo katika kata ya Mabuki. Wananchi wamehamasika na kushiriki katika shughuli mbalimbali za Maendeleo kama vile uchangiaji wa gharama za Ujenzi wa Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji katika kijiji cha Ndinga, uchangiaji wa gharama za ujenzi wa shule katika Kijiji cha Lubuga, utumiaji wa Soko la Nyashishi, Ujenzi wa Maabara Shule ya Sekondari Mamaye nk.

**Inaendelea**

8. Jumla ya watoto waishio katika mazingira hatarishi 4384 wamepati wahuduma mbalimbali, ambapo Me ni 2348 na Ke ni 2036. Huduma zilizotolewa ni pamoja na Chakula, Msaada wa Kisheria, Afya, Elimu, Makazi, Matunzo na Msaada wa Kisaikolojia. Huduma hizi zilitolewa na Shirika la MOCSO.

# Inaendelea

9. Vijana 08 vyaVijana vimepatiwa Mkopo wenye thamani ya Tsh.46,000,000/= na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Sengerema Foundation.

10. Kutoa huduma kwa Familia naWatoto. Jumla ya mashauri ya ndoa yaliyotufikia ni 81, kati ya hayo, mashauri 72 yamemalizika kusikilizwa, mashauri 05 yalipelekwa mahakamani na mashauri 04 yanaendelea kusikilizwa.

# IDARA YA UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UDHIBITI TAKA NGUMU

**Utangulizi:**

**Shughuli za idara hii zinajumuisha;**

1. Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira yaani Kelele, uharibifu wa Ardhi, Maji, hewa na udhibiti wa taka ngumu (Usafi,Usimamizi wa dampo, Uhifadhi wa taka).
2. Hifadhi ya Mazingira inajumuisha shughuli za kusimamia tathmini ya athari za Mazingira, upandaji miti, mau, upakaji rangi majengo na upendeshaji mji na bustani za mjini.

# MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

1. Kuzimba kimoja kati ya vizimba 4 kimejengwa kwa ajili ya kutunzia taka Ngumu katika Eneo la Soko Jipya.
2. Usafi wa Mazingira katika kaya na maeneo ya Biashara umeongezeka kutoka 30% 2016 hadi 66% Mwaka 2017
3. Uelewa wa Jamii juu ya umuhimu wa upandaji na utunzaji miti umeongezeka kutoka Vijiji 11 Mwaka 2016 hadi Vijiji 28 Mwaka 2017 vya Nduha, Mwambola, Isenengeja, Ibinza, Ilalambogo, Mahando, Lubili, Mwamazengo, Kabale, Gulumungu, Lukanga, Mwagimagi, Gukwa, Mbalama, Kwimwa, Lutaletale, Mwamboku, Mwamaguha, Mwanangwa, Lubuga, Ndinga, Maganzo, Magaka, Ngeleka, Matale, Kifune na Mapilinga.

# Inaendelea

4. Jumla ya wadau 2 wa Utunzaji Mazingira wamewezeshwa na kufanikiwa kupata Ufadhili wa Fedha Kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania(TaFF) kwaajili ya uanzishaji mashamba ya Miti na Ufugaji Nyuki kijiji cha Mwasonge ( Mizinga 150 na Miti 3496) na Gambajiga (miti 4386 na Hekta 12 za Ngitiri).

# Inaendelea

5. Uelewa wa Wawekezaji juu ya Uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004 umeongezeka kwa 56% kutokana na ukaguzi Mazingira uliofanyika katika viwanda vya JASCO, Sayona, KASCO, CHOBO, Miradi ya Ufugaji Samaki, Ghala la Baruti, Mradi wa Shamba la Kuku, Vituo vya mafuta, Migodi ya Wachenjuaji dhahabu 32, Wachimbaji wadogo Lubili, Busongo, Mwamazengo na wawekezaji wapya 7 waliopo maeneo ya Nyang`omango, Usagara, Isamilo, Ngudama, Misasi na Ntende.

# Inaendelea

6. Andiko moja la mradi lenye la Tsh 14,000,000 limefanikiwa na Ths 5,600,000 tayari zimeingia katika Akaunti ya H/w Development kwaajili ya Ufugaji nyuki na Utunzaji Misitu kati ya Mandiko ya Miradi 5 (Project Proposal ) yaliyotumwa kwaajili ya kuomba ufadhili katika uhifadhi wa Mazingira na kukabiliana na mabadiko ya Tabia Nchi kwa wadau mbalimbali wa maendeleo na Wizara

7. Jumla ya Migogoro 9 ya Uvamizi na Uharibifu wa Mazingira kutoka vijiji vya Misungwi, Busongo, Kigongo, Mwasonge,Mwambola, Mwajombo,Ntende,Mwanangwa na Nyamatala imesikilizwa na ufafanuzi wa kitaalamu umetolewa pamoja na kutoa Ilani ya marekebisho na Kusitisha Uvamizi wa Mto Kijiji cha Mwasonge.

# KITENGO CHA SHERIA

## UTANGULIZI

- Kitengo hiki cha Sheria kipo chini ya Idara ya Utawala. Miongoni mwa majukumu ya kitengo hiki ni:
- Kumshauri Mkurugenzi Mtendaji katika maswala yanayohusiana na sheria
- Kuwashauri wakuu wa idara, Watumishi na wananchi wa wilaya ya Misungwi kiujumla katika maswala ya kisheria
- Kumwakilisha Mkurugenzi katika mashauri ambapo ni mlalamikaji/ mwombaji au mlalamikiwa/ mujibu maombi.

# MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

Kitengo cha sheria katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 kimetekelezwa shughuli zifuatazo;-

1. Kushauri na kuapisha mabaraza ya ardhi ya kata 15(ambayo yaliyokuwa yamemaliza muda wake kwa mujibu wa sheria) na Mabaraza ya vijiji 20 yaliyokuwa yamemaliza muda wake kwa mujibu wa sheria)
2. Kuandaa Mikataba (5) na hati za makubaliano (4)
3. Kutoa ushauri wa kisheria kwa kwa wananchi na wananchi kiujumla.

# Inaendelea

4. Kuongoza mchakato wa kuanzisha **Sheria Ndogo ya Kodi ya Majengo**.
5. Mwanasheria mmoja amehudhuria mafunzo ya sheria kwa vitendo katika Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo(Law School)
6. Kusimamia na kuendesha kesi 37 za Halmashauri
7. Kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu 20 wa ushuru wa huduma,ambapo makampuni 4 wamelipa
8. Wanasheria wawili kuhudhuria semina ya utungaji sheria ndogo na uendeshaji wa mashauri ya Serikali za Mitaa

# KITENGO CHA TEHAMA

**Malengo yaliyokubalika katika Mpango kazi 2016/2017**

1. Kufunga Mkongo wa Taifa
2. Kutengeneza Tovuti ya Halmashauri
3. Kutengeneza Barua Pepe za Serikali
4. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa kielekroniki kwa kuongeza mashine za kukusanyia mapato
5. Kuweka kiambo cha mtandao wa ndani (LAN) katika vituo vine (4) vya kutolea huduma za Afya pamoja na Hospitali ya Wilaya.
6. Kuunganisha ofisi zote za Halmashauri katika kiambo cha mtandao wa ndani (LAN).
7. Kuunganisha shule zote za Serikali katika Mtandao wa Mawasiliano.
8. Kukusanya taarifa na Kuandika Habari na Makala mbalimbali za Magazeti na Luninga za maendeleo ya Halmashauri

# Mafanikio/Utekelezaji

Katika maeneo hayo ya mpango kazi, tumetekeleza na kufanikiwa katika maeneo yafuatayo;

1. Kufunga Mkongo wa Taifa (Optic Fibre) kwa gharama ya Tshs. 16,000,000/= na Mifumo mitano(5) inatumia mkongo wa Taifa, mifumo hiyo ni:

- Mfumo wa Usimamizi wa fedha za umma na malipo(EPICOR)
- Mfumo wa taarifa za kiutumishi (HCMIS-Lawson)
- Mfumo wa Mapato (LGRCIS)
- Mfumo wa kutunza na kutuma taarifa za wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari (BEMIS)
- Kuimarisha upatikanaji wa Mtandao wa Intaneti kwenye Ofisi za Idara za Elimu,Utumishi,Fedha na TEHAMA

# Inaendelea

2. Kutengeneza Tovuti ya Halmashauri , kwa ufadhili wa mradi wa PS3
3. Kutengeneza barua pepe za Serikali 22 za Idara kwa gharama ya Tshs. 840,000/=
4. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa kielekroniki kwa kununua mashine 77 hadi sasa.
5. Kuweka kiambo cha mtandao wa ndani (LAN) katika Hospitali ya Wilaya.
6. Kutoa Makala 1 ya shughuli za maendeleo kwenye Luninga ya TBC
7. Kutoa Makala 1 ya Toleo Maalum ya Shughuli za maendeleo kwenye Gazeti la Habari Leo
8. Kuunganisha ofisi za Idara 5 za Halmashauri katika kiambo cha mtandao wa ndani (LAN).

# TASAF

**MAFANIKIO 2016/2017**

1. Uhaulishaji fedha kwa walengwa 8671
2. Utekeleaji wa miradi 58 katika vijiji 50
3. Uhawilishaji fedha za ruzuku za utoaji ajira za muda kwa walengwa 7035 katika vijiji 50
4. TASAF imehakikisha watu wa asili wanapata manufaaa kiuchumi na kijamii kutokana na miradi ya utoaji ajira za muda.
5. TASAF imehakikisha watu wa asili wanapata manufaa ya Mpango kulingana na utamaduni wao kwa kuzingatia jinsia

# Inaendelea

6. Tumehamasishs wananchi kujiunga na mfuko wa bima ya afya na walengwa 6379 wamekwisha jiunga kati ya walengwa 8671
7. TASAF imehakikisha kaya maskini zinakuwa na uhakika wa kupata milo miwili hadi mitatu kwa siku
8. Tumewezesha mahudhurio ya wattoto mashuleni na cliniki kuongezeka kwa hili ni mojawapo ya masharti yanayopaswa kutimizwa na walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini.

# MAFANIKIO YA SEKTA YA UVUVI 2016/2017

1. umefanikiwa kukusanya maduhuli kupitia vyombo vya uvuvi na wavuvi Tshs 33754400/= Kwa mchanganuo ufuatao

- Leseni ya vyombo makisio Tshs 4496000/= kusanyo 7180000/=
- Leseni za uvuvi makisio Tshs 13488000/= kusanyo 20709000/=
- Mialo makisio Tshs 4320000/=Kusanyo 5865400/=Jumla Tshs 33754400/=

.

# Inaendelea

2. Tumefanya doria 49 na zana haramu zimekamatwa zenye ya sh 217780000/= na zimechomwa moto kokoro BS 127 timba MF 291 GN 3424 kokoro BOS 850 Tupa tupa CN 08 kamba 9930.
3. Elimu ya ufugaji viumbe kwenye maji imetolewa kwa wadau 150 na jamii imehamasika juu ya ufugaji samaki ambapo watu watatu wamechimba mabwa yapatayo 32 ya samaki aina ya Sato na Kambale
4. Jamii imehamasika juu ya uhifadhi wa mazari ya samaki na Uvuvi endelevu wa rasilimali ya ziwa hifadhi ya chole imeimarishwa Mwasonge, Mwalogwabagole na Lugobe zimehamasika.

# KITENGO CHA UTHIBITI UBORA WA SHULE

- Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule Wilaya ya Misungwi ilikuwa inamalengo ya kukagua shule za Msingi 70, Elimu ya Awali 70 na Elimu ya watu wazima 70 kwa kaguzi za aina tofauti. Ukaguzi wa jumla 30, Ukaguzi wa Kushtukiza 31, Ukaguzi wa Ziara 6 na Ukaguzi wa kufuatilia 3.

# Mafanikio

Katika kaguzi zilizofanyika tangu mwezi Julai 2016 hadi Juni 2017 kulikuwa na mafanikio mbalimbali ambayo ni;-

- Kukagua shule za Msingi 54, Elimu ya Awali 54 na vituo vya Elimu ya watu wazima 54 sawa na asilimia 74
- Kukagua shule maalumu zinazotegemewa kujengwa na kupata kibali cha ujenzi ni shule 2
- Kutoa ushauri kwa walimu wafundishao darasani wa shule 54 zilizokaguliwa.

# Inaendelea

- Kutoa ushauri kwa wanakamati wa shule 54 zilizokaguliwa.
- Kutoa ushauri kwa wadau wengine kwa shule zilizokaguliwa.
- Kutoa maelekezo na ushauri kuhusiana na mtaala ulioboreshwa kwa kutoa msisitizo wa kutumia vitabu,miongozo na maandalio ya masomo kutokana na mabadiliko hayo kwa walimu wafundishao shule hizo na hasa wale wa Elimu ya Awali,darasa la I, II na III.

# Inaendelea

- Kuelekeza matumizi zaidi ya maktaba kwa wanafunzi na walimu wa shule zilizokaguliwa.
- Kuhamasisha ujenzi wa maunzu ya vyoo kwa kamato za shule zilizokaguliwa.
- Kukagua shule 20 duni katika mtihani wa Taifa wa darasa la 7 uliofanyika mwaka 2016.
- Kukagua shule 30 zilizokuwa kwenye utepe mwekundu na njano katika matokeo ya mtihani wa kitaifa kwa darasa la VII mwaka 2016.
- Kukagua walimu waliothibitishwa kazini mwaka 2017 walimu wapatao 147.

# KITENGO CHA BIASHARA

## Utangulizi

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 kitengo cha biashara kimetekeleza majukumu yake kwa mjibu wa Sheria kanuni na taratibu kama ifuatavyo:-

# Mafanikio

- Kwa mjibu wa Sheria Na 25 ya 1972 ya Leseni za biashara, Kitengo kimeweza kuwasajiri wafanya biashara na kuzirasimisha biashara zao ambapo katika zoezi hilo biashara 933 zimesajiriwa na kurasimishwa kwa kupatiwa leseni za biashara. Katika kusimamia sheria hiyo kumekuwa na ongezeko kubwa la watu kujiunga na sekta hiyo kwa ajiri ya kukuza uchumi wao binafsi na wa taifa kwa ujumla. Katika urasimishaji huo kitengo kimekusanya ada za leseni Tsh. 45,013,853/=

# Inaendelea

- Kwa mjibu wa Sheria ya Usafiri na usafirishaji na kanuni zake (The motorcycle and tricycle regulation of 2010) kitengo kimekusanya kiasi cha Tsh. 1,796,000/=. Na vijana wengi wamejiajiri katika sekta hiyo ya usafirishaji abiria kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili na matatu.
- Kwa mjibu wa Sheria ndogo za mapato ya soko – jipya Kitengo kimesimamia vema uendeshaji wa soko hilo na kukusanya mapato (ushuru) na kiasi kipatacho Tsh. 16,200,000/=. Wafanya biashara wadogo na wa kati wapatao 142 wanaendelea na shughuli zao za kiuchumi katika soko hilo.

# Inaendelea

- Kwa mjibu wa Sheria ya vileo (The liquor licensing Act No. 28 of 1972 kitengo kimekusanya Tsh. 3,308,000/=
- Kwa mjibu wa Sheria ya Hotel, Hotel leavy Act kitengo kimeweza kukusanya kiasi kipitacho 6,629,700/=

  Kwa hiyo Kitengo kimeendelea kutekeleza majukumu yake, kwa maana ya kusimamia sheria za uendeshaji biashara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuweza kukusanya jumla ya Tsh. 73, 517,853/= kwa mchanganuo ufuatao;-

# Jedwali Na.1: Mchanganuo wa Mapato kwa mwaka 2016/17.

| Na | Chanzo | Mapato<br>July-June 2017 | %<br>ya utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada za Leseni za biashara | 45,013,853/= | 71.45% |
| 2 | Hotel leavy | 6,629,700/= | 73.6% |
| 3 | Ushuru wa soko jipya | 16,200,000/= | 80% |
| 4 | Leseni za vileo | 3,308,000/= | 77.7% |
| 5 | Leseni za Pikipiki | 1,796,000/= | 112.25% |
| | **JUMLA** | **73,517,853/=** | |

# KITENGO CHA USHIRIKA

- Vijana wamehamasika kujiunga kwenye vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo (SACCOS) kwa ajili ya kupata mikopo yenye riba nafuu na kujiwekea Akiba na Amana zao hususani Misungwi Vijana SACCOS.
- Baadhi ya vyama vya Ushirika AMCOS na SACCOS wamepata Elimu ya Utunzaji wa vitabu vya mahesabu na kwa sasa wanauwezo wa kuandika vitabu na kufunga hesabu zao wenyewe.
- Vyama vitatu vya Ushirika wa Akiba na Mikopo wamepata Hati safi ya hesabu zao (Unqualified Opinion) kwa mwaka 2016 vyama hivyo ni Mkukuwami,Ukiriguru Kilimo na Usagara Parish SACCOS na hivyo kujenga moyo wa Imani kwa wanachama kuhusu usalama wa fedha zao.

- Vyama vya Ushirika vinakopesheka kwenye Asasi za kifedha mfano; Mkukuwami SACCOS walipata mkopo wa Tshs.300 milioni kutoka Benki ya CRDB na Ukiriguru – Kilimo walipata Tshs.100 milioni.
- Vyama vya Ushirika vimeweza kutoa nafasi za ajira kwa vijana, kwenye nafasi za utendaji, kwa Misungwi vijana SACCOS vijana 2 wameajiriwa, Mkukuwami SACCOS vijana 4 na Ukiriguru – Kilimo vija 2.

# IDARA YA MIPANGO

## KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17 IDARA YA MIPANGO ILIPANGA KUTEKELEZA KUSIMAMIA MALENGO YAFUATAYO

| LENGO PANGWA | SHUGHULI PANGWA | MAFANIKO |
|---|---|---|
| Kuhakikisha Mfumo wa Ukaguzi na ufuaatiliaji wa Miradi yote ya Maendeleo unimarishwa kuanzia asilimia 40 hadi asilimia 75% katika Ngazi za vijiji , Kata na wilayani ifikapo 2019. | Kufanya Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta za Elimu Msingi, Elimu Sekondari, Afya, Kilimo, Maji, Maendeleo ya jamii , Ujenzi, Utawala, Mifugo , Mazingira, Nyuki na Uvuvi | Timu ya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya Maendeleo ambayo inahusisha Idara ya Mipango, idara ya ujenzi, Afya, Maji, Kilimo na Ugavi Imeundwa. Timu hii imeweza kukagua miradi yote kwa kila Hatua na kumshauri mkurugenzi Mtendaji pale ambapo kuna Mapungufu, Aidha Taarifa za robo 4 za utekelezaji wa miradi kwa mwaka husika zimeandariwa kikamilifu kwa asilimia 100 na kuwasilishwa ngazi ya Mkoa. **Miradi iliyoweza kukaguliwa na kuandikiwa Taarifa ni kama** |

## a) Miradi ya Ruzuku ya Maendeleo (LGDG)

- Ujenzi wa Jengo la Utawala Shule ya Sekondari Gulumungu Mradi huu Umekamika kwa Asilimia 85%
- Ujenzi wa nyumba ya Mganga Zahanati ya Gambajiga ujenzi huu umekamilika kwa 100%
- Ujenzi wa nyumba ya Mganga zahanati ya Bugisha umekamilika kwa Asilimia 75%

- Ujenzi wa kituo cha Afya Kata ya Mondo Boma limekamilia kwa asilimia 100% hatua inayo fuata ni kufunga lenta na kuweka matofali ya kozi za juu baada ya kufunga Lenta.
- Ukamilishaji wa ujenzi wa vyoo katika shule 13 umekamilika kwa Asilimia 55% na ujenzi bado unaendelea baadhi ya vyoo.
- Ujenzi wa ofisi kata ya Mwaniko umekamilika kwa 100% bado kukabidhiwa lengo ni kutoa huduma bora

- Ujenzi wa ofisi ya Kata ya Fella umekamilika kwa asilimia 85% lengo ni kutoa huduma bora kwa wananchi.
- Ujenzi wa choo  na mabafu  katika stand ya mabasi  Misungwi  umekamilika kwa asilimia 70%.lengo ni kuongeza mapato ya Halmashauri
- Ujenzi wa Machinjio usagara  Umekamilika kwa Asilimia 55%

- Ujenzi wa Machinjio ya Misungwi umekamilika kwa asilimia 40%
- Ujenzi wa stand ya mabasi madogo Usagara umekamilika kwa asilimia 75% kazi inaendelea lengo ni kuongeza mapato ya Halmashauri

- Aidha idara imeweza kuratibu ukaguzi wa Miradi ya ukarabati wa Vyoo katika shule za Msingi 13 za Mwasagela Mwambola, Masawe, Lukelege, Mwakiteleja, Ibongoya A, Gulumumungu, Nyalugembe, Busegeja na Nyashitanda , ukamilishaji wa vyoo hivi upo Hatua mbalimbali

- Ununuzi wa vifaa vya ofisi ambavyo ni Generator lenye ukubwa wa KV 12.hivyo tatizo la Umeme halitasumba tena mara umeme utakapokatika kazi za ofisini hazitasimama,
- Komputa 2 na printer 1 coloured na yenye scanner zimenunuliwa na zinatumika.

# b) Miradi ya maombi Maalumu

- Ujenzi wa madarasa 6 na ofisi 3 za walimu katika shule maalum za Misungwi, Busagara, na Kigongo yamejengwa na yamekamilika kwa asilimia 100% bado kukabidhiwa.

- Ukamilishaji wa fensi ya mitindo shule ya Msingi umefanyika kwa asilimia 90 hii ni pamoja na kuweka umeme, Hivyo ulinzi kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi unaendelea kuimarika

- Ukarabati wa bwalo na jiko katika shule ya msingi Mitindo unaendelea kufanyika na umefikia asilimia 60%

- c) **Miradi mingine** ambayo imekaguliwa na kuandikiwa ripoti ya Ukaguzi ni Miradi ya barabara,Daraja la Isenengeja,ujenzi wa Hosteli S/M Mitindo,Ujenzi wa madarasa 5 na ofisi 1 shule ya Msingi Mitindo yameanza Kutumika, Ujenzi wa Madarasa 4 na Ofisi 1 Shule ya Msingi Mbela yamekamilkka na yanatumika.

- Timu ya ya Assessment ya wilaya yenye jumla ya Wajumbe 12  kutoka Katika idara za Utumishi, Mipango, Fedha, M/Jamii, Maji, Afya, Ugavi, Elimu Msingi, Elimu Sekondari na Kilimo imeundwa.Timu hii imeweza kutoa elimu kwa kamati zote za maendeleo ya kata  (WDC) 27 juu Mfumo Mpya wa Upatiwaji wa fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo (LGDG)  na O & OD iliyoboreshwa,Shughuli hii imefanyika Kwa asilimia 90 ambapo kata 27 zote zimeelimishwa na jitihada za wa wananchi  juu ya miradi mbalimbali ya maendeleo  ya wananchi kwa  miradi waliyoanzisha tayari kwa nguvu zao  katika vijiji zimeiburiwa .

- Ziara za Mkurugenzi Mtendaji juu ya kukagua shughuli za maendeleo katika kata 13 kwa taasisi zote Katika sekta zote zimefanyika kwa asilimia 100 ambapo miradi kadhaa iliyokuwa imesimama imewekewa mikakati ya kufufuliwa hususani mradi wa maji wa umwagiliaji kata ya Mbarika ,mradi wa Maji wa kisima Usagara na Sanjo

# Kuhakikisha mfumo wa uandaaji wa Taarifa  za utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaimarishwa kutoka Asilimia 40% hadi 75 % ifikapo 2019

- Kushirikisha idara 15 na vitengo 4 katika kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Taarifa za kila mwezi zimefanikiwa kuandaliwa na kuwasilishwa katika ngazi ya Mkoa. Aidha Taarifa za miradi za kila robo mwaka kwa robo zote 4 na Takwimu kutoka idara zote 15 na vitengo vyote 4 zimeandaliwa kikamilifu na kuwasilishwa katika vikao vya kisheria, Mkoani na Tamisemi kwa asilimia 100.

- Mpango wa bajeti ya mwaka 2017/18 umeandaliwa kikamilifu kwa asilimia 100 .Mpango huu umepitishwa katika vikao vyote vya kisheria vikiwemo kikao cha Wadau wa maendeleo(dcc),RCC , baraza la Wafanyakazi nabaraza maalumu la Madiwani Aidha umewasilishwa na kuidhinishwa na Bunge Tukufu la Jamhuri y muungano Wa Tanzania hadi sasa umeanza kutumika.

- Mpango Mkakati wa Halmashauri wa Wilaya ( SP) wa Miaka Mitano 2017/18-2021/22 ambayo ndiyo dira kuu ya Halmashauri unaoendana na mpango wa Serikali wa Miaka 5 awamu ya Pili, umeandaliwa na umekamilika na unatumika.
- Wasifu wa kijamii na kiuchumi wa halimashauri ( District social Economic Profile umefanyiwa mapitio) n a kazi hii imekamilika asilimia 95 chini ya Usimamizi wa ofisi ya Taifa ya Takwimu nbs

## Kusimamia maandiko ya miradi na kuyawasilisha ngazi mbalimbali ambapo halmashauri imefanikiwa kupata:

- Mradi wa kisima cha maji shule ya Msingi Mitindo Kisima hicho kimechimbwa nawanafunzi wanapata maji safi na salama shule ya Msingi Mitindo
- Mradi wa Matenk ya Maji Shule ya MsingI Mitindo ,Matank hayo yanatoa maji safi na Salama muda wote

- Mradi wa kuchimba kisima kupitia compassion katika kata Ya Usagara.hatua iliyopo ni kuchimba kisima hicho.
- Mradi wa kusimika Nguzo za umeme kuanzia kisesa hadi Kwenye Mradi wa Maji Fella. Nguzo hizo zimeishasimikwa  na badala ya kupampu maji kutoka kwenye chanzo kwenda katika tank kwa kutumia diseli sasa wananchi watatumia Umeme.

# Idara ya Utawala Rasilimaliwatu

# UTANGULIZI

- Idara ya Utawala Bora ni moja kati ya Idara na Vitengo 19 vya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Idara hii inashughulikia ukuzaji wa utawala bora kwa kuzingatia majukumu na malengo mkakati ya Halmashauri.

- Idara ya Utawala na Rasilimali watu ina jumla ya watumishi 160 wakiwemo Mkurugenzi Mtendaji 1, Maafisa Utumishi 3, Watunza Kumbukumbu 9, Makatibu Muhsusi 11, Wahudumu wa Ofisi 7, Madereva/fundi wa awali 14, Watendaji wa Vijiji 90, Watendaji wa Kata 20 na walinzi 5, Watumishi hawa wanafanya kazi za kuhudumia wananchi kwa ujumla, pamoja kuhudumia Idara nyingine 12 na vitengo 6 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya

# Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa na Malengo 09 ya utekelezaji (makubwa yakiwa ni

- kuhakikisha misingi ya utawala bora inaimarishwa kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata na Halmashauri kwa kuhimiza uwazi na uwajibikaji, ushirikishwaji wa wananchi kuhakikisha vikao vyote vya kisheria vinafanyika katika ngazi zote ambazo ni vikao vya Serikali za vijiji, mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, vikao vya Halmashauri na Baraza la Madiwani. Kuongeza utoaji huduma kwa kuhakikisha kuwa maabukizi ya Ukimwi yanapungua na kuimarisha uwajibikaji unaozingatia misingi ya kupambana na kupiga vita Rushwa

- Malengo yalivyoainishwa hapo juu, ndiyo yanayosimamia utengenezaji wa vipaumbele vya idara ya rasilimaliwatu na utawala na hatimaye kutengeneza Mpango-Kazi katika Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) na hatimaye mpango kazi (Action Plan). Pamoja na jukumu la kuimarisha utawala bora Idara hii inashughulikia Ajira na Nidhamu, Matumizi Mabaya ya Madaraka na Mafao ya Kustaafu.

- **Malengo ya Idara kwa mwaka wa fedha 2016/2017**
- Ili kutekeleza mpango mkakati wa Idara, Idara iliweka shughuli zifuatazo katika mpango kazi wake kwa mwaka wa fedha 2016/17

| LENGO | SHUGHULI | MALALAMIKO | YALIVYOSHUGHULIKIWA | MAFANIKIO |
|---|---|---|---|---|
| kuhakikisha misingi ya utawala bora inaimarishwa katika ngazi zote za utawala: (Kijiji, Kata na Wilaya) | Hadi kufikia tarehe 30 mwezi Juni, 2017 Idara ilikuwa ina jumla ya malalamiko **64** kati ya hayo, malalamiko 40 ni ya mwaka wa fedha 2015/2016. Malalamiko haya yalihusu matumizi mabaya ya madaraka, Ajira na nidhamu pamoja na Mafao ya watumishi wa Umma | Hadi kufikia tarehe 30 mwezi Juni, 2017 Idara ilikuwa ina jumla ya malalamiko **64** kati ya hayo, malalamiko 40 ni ya mwaka wa fedha 2015/2016. Malalamiko haya yalihusu matumizi mabaya ya madaraka, Ajira na nidhamu pamoja na Mafao ya watumishi wa Umma | Katika mwaka wa fedha 2016/17 Idara ilifanya uchunguzi wa malalamiko yote 64 (24 mapya na 40 ya zamani), na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, | Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Idara imehitimisha uchunguzi na kufunga malalamiko **57** kwa sababu mbalimbali. Malalamiko **40** yalipatiwa suluhu na watumishi na wahusika kupewa haki zao |

# Inaendelea

| LENGO | SHUGHULI | MALALAMIKO | YALIVYOSHUGHULIKIWA | MAFANIKIO |
|---|---|---|---|---|
| | | Mambo yaliyolalamikiwa ni: Kutolipwa malimbikizo ya mishahara, Kutopadishwa vyeo watumishi, Kucheleweshewa mafao ya kustaafu, Kutorejeshwa kwenye daftari la pensheni, nauli na gharama za mizigo baada ya kustaafu, kubadilishwa kada, Kutopewa uhamisho pamoja na watumishi kucheleweshewa kulipwa madai/stahiki zao | Idara ilikuwa imefanikiwa kuhitimisha uchunguzi wa malalamiko 50, na hivyo kubaki na malalamiko 14 yanayohusu utovu wa nidhamu. Idara imefanya uchunguzi wa malalamiko hayo kwa njia mbalimbali, kama vile mawasiliano ya barua, uchunguzi wa hadharani, na kuwafuata walalamikiwa kwenye ofisi zao. | Malalamiko **04** yalifungwa kwa wahusika kushindwa kuthibitisha madai yao na idara kutokuwa na mamlaka ya chunguza na baadhi ya walalamikaji kushindwa kutoa ushirikiano, Watumishi **13** kupewa ushauri wa namna ya kushughulikia madai yao |

| LENGO | SHUGHULI | MALALAMIKO | YALIVYOSHUGHULIKIWA | MAFANIKIO |
|---|---|---|---|---|
| | Kuhamasisha uzingatiaji wa misingi ya utawala bora miongoni mwa viongozi, jamii, pamoja na kusimamia vikao vya kisheria vya Halmashauri | | Shughuli hii ilifanywa kutokana na matokeo ya Uchunguzi wa Hadharani wa Idara wa mwaka 2016 uliooneshа kuwa kuna ukiukwaji mkubwa wa utoaji wa huduma kwa misingi ya utawala bora pale mamlaka za serikali za vijiji zinaposhindwa kusoma mapato na matumizi | Kuanzia tarehe 23/9/2016, Idara ilifanya mikutano ya hadhara na watendaji, viongozi na wananchi katika Kata (17) za Wilaya ya Misungwi ili kutoa miongozo kwa Watendaji wa ngazi za Vijiji na Kata kuhusu uzingatiaji wa misingi ya utawala bora katika masuala ya ardhi |

| LENGO | SHUGHULI | MALALAMIKO | YALIVYOSHUGHULIKIWA | MAFANIKIO |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Vijiji vilivyofikiwa ni Fullo, Nyabumhanda, Songiwe, Kabale, Seeke, Buhingo, Willi, Ukiriguru, Mwagala, Ngereka, Nyamatara, Nyang'olongo, Nyabusalu, Mwakiteleja, Mwagimagi, Gukwa, Ihelele, Fella, Mwaholo, Sumbuka, Budutu, Kanyelele, Gambajiga, Mwasubi, Lukelege, Mwanenge na Koromije. Aidha vilifanyika vikao 12 vya Fedha Uongozi na Mipango, Vikao vine vya Baraza la Madiwani na Vikao vitatu kwa kila idara na Kitengo cha Halmashauri. |

- **Pamoja na shughuli na mafanikio zilizotajwa katika jedwali kwa kipindi cha Mwaka 2016/2017 imesimamamia maslahi na stahiki mbalimbali za kisheria za watumishi kama vile.**

- Kusimamia nidhamu na maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni za Maadili ya Madiwani kwa kipindi chote cha mwaka 2016/2017 pamoja na kusimamia stahiki za kisheria za watumishi wa umma kama vile Mishahara, posho, matibabu, likizo, masomo, Kusimamia na kuandaa/kushughulikia maslahi ya Wah. Madiwani kama vile posho za vikao na posho za mwezi.

- Kusimamia kwa kushirikiana na Wakuu wa Idara/Vitengo kuhakiki watumishi (Staff Audit) na kuondoa watumishi wote wasiostahili kulipwa mishahara kwa sababu mbalimbali kama vile kufariki, kuacha/kuachishwa kazi, utoro, kustaafu, kufungwa pamoja uhakiki wa vyeti vya masomo na taaluma za watumishi. Kwa kufanya hivyo idara imewafuta watumishi 142 kutokana na sababu mbalimbali kwa kipindi 2016/2017 kama inavyoainishwa: Wastaafu 40, Vyeti feki 78, Utoro 07, Kifo 04, utovu wa nidhamu 07 na waliojiudhuru 08. Aidha idara imekamilisha uhamisho wa watumishi 13 kwenda Halmashauri mbalimbali, kupokea watumishi 12 kutoka Halmashauri na taasisi mbalimbali na Watumishi 10 wa ajira mpya (walimu 08 madaktari 02)

- Kushughulikia ujazaji na kuingiza kwenye mfumo wa Taarifa za watumishi na Mishahara (HCMIS) fomu za watumishi wote, kushughulikia ujazaji wa fomu za Uadilifu na MWAMTUKA yaani OPRAS.
- Kushughulikia mafao ya watumishi wastaafu, mirathi na walioacha kazi kwa kushirikiana na mifuko ya pensheni LAPF, PSPF, NSSF na Hazina.

# CHANGAMOTO, MAPENDEKEZO NA MATARAJIO

**Changamoto**

- Idara ya Utawala katika kutekeleza majukumu yake inakabiliana na changamoto zinazorudisha nyuma mipango iliyojiwekea na kupunguza ufanisi wa kazi kama inavyoelezwa kwenye mpango kazi wa Idara. Baadhi ya changamoto hizo ni:

- Changamoto ya kwanza ni ukosefu wa rasilimali fedha unaosababisha kutokamilika au kutekelezwa kwa baadhi ya kazi zilizokuwa katika mpango kazi wa Idara wa mwaka 2016/2017.
- Changamoto ya pili ni mfumo wa mawasiliano (internet) kuwa duni hali inayosabisha wateja kupata huduma isiyoridhisha (au wakati mwingine mawasiliano kukosekana kwa muda nmrefu).

- Changamoto ya tatu, ni upungufu wa vitendea kazi. Idara ya Utawala inaupungufu mkubwa wa vitendea kazi kama vile kompyuta za kufanyia na "printers" pamoja na Scanner. Idara hii ina Scanner moja ambayo hata hivyo inafanya kazi chini ya kiwango.

- Changamoto nyingine ni kutokuwepo kwa ofisi za kutosha za  la utawala, hali inayopunguza ufanisi katika utendaji kwa kutokuwa na ofisi za kutosha

**Mapendekezo**

- Idara ya Utawala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kukakabiliana na changamoto zilizojitokeza. Baadhi ya mambo yafuatayoyanatakiwa nyatakelezwe:

- Upatikanaji wa fedha za kutosha katika mpango kazi wa Idara wa mwaka wa fedha 2017/2018.
- Upatikanaji wa mfumo ulio thabiti utakaoowezesha kutoa huduma sahihi na kwa muda sahihi.
- Kuongezeka kwa vitendea kazi ili kurahisisha utoaji huduma kwa haraka na yenye tija kwa wateja.
- Kupatikana kwa ofisi/vyumba vya kutosha kwa maafisa rasilimaliwatu ili kujenga usiri kwa mteja/wateja anapohudumiwa

# Matarajio Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018

- Idara ya Utawala itaendelea kupokea malalmiko mapya na kuyafanyia kazi malamiko ya zamani kama ilivyoainishwa kwenye mpango kazi wa idara.
- Maafisa wa Idara ya Utawala kwa kushirkiana na Waheshimiwa Madiwani kutembeleaTaasisi za Serikali pamoja na Taasisi Binafsi zinazolalamikiwa na wakuu wa Taasisi hizo ili kutatua malamiko ya watumishi (Wastaafu) na kuyapatia ufumbuzi kwa haraka na kwa wakati

- Kutoa elimu kwa kutumia njia mbalimbali kama redio, luninga, vipeperushi na majarida pamoja na kuyafikia maeneo yanayoathiri utawala bora kadri fedha zitakavyoruhusu.
- Kuandika andiko mradi ”proposal” ili kupata fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo watakao saidia utekelezaji wa majukumu ya idara kama yalivyoainishwa kwenye mpango mkakati

# IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

| Na | Lengo | Mafanikio kazi zilizofanyika kwa takwimu na sailimia |
|---|---|---|
| 1 | Kuongeza ufanisi katika Kusimamia mapato na matumizi ya fedha kwa kuzingatia sheria na taratibu kutoka 65% hadi 87% ifikapo June 2020 | Halmashauri imeweza kusimamia mapato na matumizi kwa ufanisi na hivyo kupata Hati safi ya ukaguzi wa Hesabu kuishia June 2017 |
| 2 | Kuongeza mapato ya ndani kutoka asilimia 80% hadi 99% ifikakapo June 2020 | Halmashauri imewezesha matumizi ya Mfumo wa kukusanyia mapato kwa njia za kielektroniki sambamba na kuboresha (takwimu) database za wafanyabiashara, majengo, mabango na Minara yote yaliyopo ndani ya Mamlaka ya Wilaya |

| Na | Lengo | Mafanikio kazi zilizofanyika kwa takwimu na sailimia |
|---|---|---|
| | | •Ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato kutoka mashine 15 hadi mashine 77<br>•Hadi kuishia June Halmashauri imeweza kukusanya kiasi cha Shs 1,331,077,446.11 Sawa na asilimia 83.12 ya makisio ya Shs. 1,601,368,000 ya mwaka 2016/2017 |